

## Ubainikaji wa Mahusiano na Mamlaka kupitia Usemi kwenye Nyumba za Watawa za Malezi

*Teresia W. Waweru, John Habwe na P.I. Iribemwangi  
Chuo Kikuu cha Nairobi*

### Ikisiri

Utafiti huu unahusu kujieleza na ubainikaji wa mahusiano na mamlaka yanayoweza kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye nyumba za watawa za malezi katika kanisa Katoliki nchini Kenya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sarufi amilifu msonge ya Michael Halliday (1985). Data ya uchunguzi ya utafiti huu ilikusanywa kutoka nyanjani katika nyumba za malezi mjini Mombasa ambapo lugha ya Kiswahili hutumika kwa kiasi kikubwa na ni mojawapo ya lugha kuu za mawasiliano. Matini zilizoangaziwa zilikuwa katika kiwango cha kishazi na sentensi. Maswali matatu yaliyopaniwa kujibiwa na makala haya ni kwamba je, lugha hutumiwa vipi kati ya walezi na walelewa wakati wa kujieleza. Pili, je mamlaka hubainikaji vipi kwenye mawasiliano katika nyumba za watawa za malezi? Tatu je, mamlaka na mahusiano hudhihirika vipi katika matumizi ya lugha iliyo rasmi na isiyo rasmi katika nyumba za watawa za malezi? Matokeo ya utafiti yanatanaonyesha kuwa kujieleza na ubainikaji wa mahusiano na mamlaka yasiyo wazi kati ya walezi na walelewa hudhihirika katika usemi katika nyumba za watawa kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**Maneno Muhimu:** *Namna, Mahusiano, Vitenzi Leksika, Walelewa, Walezi*

### Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Katika nyanja na miktadha mbalimbali za kijamii, lugha huwa kiungo muhimu kinachotumiwa na wasemaji kuwezesha mawasiliano na utangamano unaopaswa kuwoko katika usemi na mahusiano ya kimamlaka. Itakumbukwa kuwa kanisa Katoliki ni mojawapo ya asasi za kibinadamu zilizo na desturi, na kudhihirisha namna. Hivyo, namna ni kipengele muhimu cha kujadili na kukielewa kupitia matumizi ya lugha na ukuzaji wa mahusiano na mamlaka katika nyumba za malezi.

Watawa ni mojawapo ya kiungo muhimu cha kanisa Katoliki. Uongozi katika kanisa Katoliki hutekelezwa kuzingatia ngazi mbalimbali za kiutawala kama vile mama mkuu, makamu wake, wasaidizi wa mama mkuu, viongozi wa maeneo na walezi. Kuna watawa pia walioweka na kujifunga na nadhiri za daima, nadhiri za muda pamoja na walelewa. Usemi husaidia kuwelewa muktadha wa kile kinachozungumziwa na hukuza uhusiano kati ya msikilizaji na mzungumzaji. Muktadha wa kile kinachozungumziwa kwenye nyumba za watawa za malezi unaweza kuitumia lugha katika usemi kupitia kujieleza na kubainika kwa mamlaka.

Kama anavyoelezea Fairclough (1989, 2010), dhamira na namna ni muhimu kwa kuwa swali kuhusu wanachojihusisha nacho wakati wanapotoa kauli fulani kama vile kuuliza maswali, kutoa amri, kushauri au hata kutoa maelekezo ni muhimu na huchangia katika uundaji na uhifadhi wa mahusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji kama ilivyo kati ya mlezi na mlelewa. Dhamira huchangia katika nafasi ambayo mwandishi au mzungumzaji huchagua katika tukio la usemaji na majukumu anayompa msikilizaji. Ikiwa mzungumzaji kwa mfano ataamua kutumia dhamira ulizi, anachukua jukumu la yule anayeuliza maswali na msikilizaji katika nafasi ya yule anapaswa kuyajibu maswali hivyo kumfanya mzungumzaji kuonekana kama mwenye mamlaka dhidi ya msikilizaji. Dhamira, sio muhimu tu kwa kutafuta ni mawazo gani yanatiliwa mkazo au yasiyotiliwa mkazo katika usemi fulani lakini pia katika kudhihirisha jinsi watu wanavyojitambulisha na kujipatia nafasi katika usemi husika.

Namna inahusiana na uamuzi kati ya 'ndio' na 'la' ambayo inaeleza aidha hukumu ya mzungumzaji isiyo na upendeleo kuhusu kinachozungumzwa au katika kuonyesha mahusiano ya

kijamii, mahusiano ya kimamlaka na viwango vya urasmi. Ni mtazamo wa mzungumzaji au mwandishi kuhusu ulimwengu na ni muhimu kwa kuangalia mahusiano ya kimamlaka kwa kuwa kupitia namna kuna uwezekano wa kujua kwa mfano ni dhana zipi zinazotiliwa mkazo na zisozotiliwa mkazo. Endley (2010) anaeleza kuwa namna hutoa mtazamo wa mzungumzaji kuhusu tukio linaloelezwa. Uchunguzi huu hata hivyo umejikita zaidi katika kipengele cha namna ambacho ni cha kimsingi katika kuangalia mahusiano ya kimamlaka.

### **Msingi wa Kinadharia**

Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu Msonge iliyoasisiwa na kuendelezwa na Michael Halliday (1976, 1985, 1994, 2004). Nadharia hii inajihusisha zaidi na wazo la uamilifu wa lugha na maana kama uteuzi wa jinsi lugha au mfumo wowote wa kisemiotiki unavyoelezewa kama mfumo uunganishao uchaguzi na uteuzi kama njia ya kuleta maana. Aidha, hujihusisha na muundo wa kisintaksia. Huangalia uamilifu wa lugha kama ulio muhimu sana (kile lugha inachokifanya, na namna inavyokifanya) kwa kuzingatia mielekeo ya kimuundo ambayo huziweka elementi za lugha na mifumo yake kama yenye umuhimu mkubwa. Huanza kwa muktadha wa kijamii, na huangalia jinsi lugha huyashughulikia majukumu yake, jambo ambalo hulazimishwa na muktadha wa kijamii. Nadharia ya Sarufi Amilifu Msonge huchukulia lugha kama mseto wa mifumo ulio na maana yenye nguvu ambayo watumiaji huiwasilisha kupitia kufanya uamuzi kutoka kwa uchaguzi mbadala. Maamuzi ya kisarufi na mikakati mingine ya usemi kawaida kufuatia nadharia hii husimbikwa katika kuonyesha nafasi ya walezi na walelewa kama watendaji wa jamii na wanaopewa nafasi tofauti za uajenti katika uelekezi (Halliday, 1985).

Uelekezi ni dhana mojawapo muhimu ya kisemantiki inayodhamiria kuweka wazi jinsi tendo linavyofanyika, anayelifanya, na analifanya kwa nani. Ni sehemu ya jukumu la kidhana la lugha na hivyo kigezo muhimu katika uchanganuzi wa ujielezaji na ubainikaji wa mahusiano na mamlaka katika usemi kupitia namna katika nyumba za malezi. La muhimu ni kuwa miundo muhimu ya kijamii huhitaji aina mbalimbali za uelekezi. Kishazi hutumiwa kuwasilisha matukio na mifanyiko ya namna mbalimbali. Katika mtazamo wa Sarufi Amilifu Msonge wa Halliday (2004), lugha ni malighafi ya kujenga maana na maana hupatikana katika uteuzi wa mitindo fulani maalum. Ili msikilizaji aweze kuipata maana, hujaribu kuelewa kile ambacho msemaji alinuia kukisema au kuelewa maana ya vipengele vya kisarufi vilivyoteuliwa na msemaji.

Mawazo ya Nadharia ya Sarufi Amilifu Msonge yalituongoza katika kuchunguza dhana ya kujieleza na ubainikaji wa mahusiano na mamlaka yanayoweza kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hili lilifanyika katika Kanisa Katoliki kwenye nyumba za watawa za malezi za shirika la masista wa Mtakatifu Yosefu wa Mombasa kupitia namna wakati wa mawasiliano kati ya walezi na walelewa katika shughuli rasmi na zisizo rasmi. Lengo lake likiwa kuangalia majukumu ya lugha yanavyotekelezwa kupitia matumizi ya lugha kwenye nyumba za malezi mjini Mombasa ambapo kuna mahusiano ya kijamii yenye mamlaka.

Mahusiano haya yanahitaji kuiunganisha jamii kupitia lugha. Utafiti ulivitumia vipengele vya kisarufi kuchunguza namna katika kuangalia jinsi lugha inavyotumiwa kudhihirisha mahusiano ya kimamlaka yanayotarajiwa kuwa yamefichwa kati ya walezi na walelewa na kuonekana kama jambo la kawaida mawazo yanayofanana na ya (Fairclough 1989, 2000, 2010).

### **Kujieleza na Ubainikaji wa Mahusiano na Mamlaka katika Usemi Kupitia Namna**

Majukumu ya kiuamilifu yanahusu matumizi ya lugha katika kuelezea mahusiano ya kijamii na ya kibinafsi (Halliday, 1985). Uchunguzi wa namna ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa swali kuhusu kile watu wanachojifunga kwake wakati wanatoa kauli, kuuliza maswali, kutoa amri, kushauri au hata kutoa maelekezo ni muhimu katika uundaji na uhifadhi wa mahusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji (Fairclough 1989, 2010; Francis na Kramer-Dahl 1992).

Kulingana na Kreidler (1998), *namna ya wajibu* ni aina ya namna yenye umuhimu wa mtu kufanya au kutofanya kitu kwa njia fulani. Inadhihirisha iwapo kauli inayotolewa ni amri, ni ya lazima,

kushauriwa au ya kuruhusiwa kulingana na baadhi ya ufahamu wa kidesturi wa awali kama vile sheria, maadili, ukawaida na kadhalika. Aina hii ya namna inadhihirisha uamuzi wa mzungumzaji kulingana na wajibu (kimaadili au kijamii), ruhusa au makatazo pamoja na hamu ya mzungumzaji kwenye kauli anayoitoa. Vitenzi hubeba maana inayohusiana na uwezo na matamano ya kuongoza mambo.

Halliday (1971) anaeleza kuwa mzungumzaji hutumia lugha kama njia ya kuingia katika tukio la mazungumzo: uelezaji wa maoni, mitazamo na tathmini, na pia wa uhusiano anaouweka kati yake na msikilizaji; na kwa njia ya pekee nafasi ya mawasiliano ambayo anayapanga ya kufahamisha, kuuliza maswali, kusihi na mengineyo. Uhakiki huu ulielekezwa na madai haya na unayatumia kuchunguza jinsi mahusiano na mamlaka ya jamii yanavyoweza kuelezewa na kubainika kupitia namna. Namna inahusu maoni au hukumu ya mzungumzaji kuhusu yanayozungumzwa au tukio la usemi katika kishazi. Uchunguzi wa namna unaonyesha umuhimu wake katika mahusiano ya kimamlaka kwa kuwa kupitia namna mtu anaweza kwa mfano kujua ni dhana zipi zinazokaziwa au kutokaziwa kuhusu mamlaka.

Namna inahusiana na uamuzi kati ya 'ndio' na 'la' ambayo inaelezea aidha hukumu ya mzungumzaji isiyo na upendeleo kuhusu kinachozungumzwa au kuonyesha mahusiano ya kijamii, mahusiano ya kimamlaka na viwango vya urasmi. Inahusiana na utoaji wa maoni au hukumu ya mzungumzaji kuhusiana na muktadha na jukumu la usemi katika kishazi (Halliday, 1994). Utafiti huu unachunguza jukumu la kimahusiano la lugha kupitia namna kwa kujadili jinsi namna inavyodhihirika katika kishazi kupitia mahusiano na mamlaka ya kijamii katika nyumba za malezi za kitawa. Hebu tuangalie mfano ufuatao unaosemwa na mlezi,

1. Hayo mambo hatutaki, tunaewana? Ndio, hayo mambo hatutaki... Tunapaswa kuchukuliana sisi sote sawa, si ati kwa sababu wewe ni Mtaita unataka kukaribia sista mlezi na unajua kuna tatizo lingine; kuna watu ambao wakikaa katika kikundi kama hiki wanataka kupendwa... si mwawajua? Ndio, Hata sekondari si mnajua? Mtu siku zote sista nikusaidie nini? Hakuna kujipendekeza kwa sista ati unajipeleka ndio ukaseme wengine, ama ndio akupende, hayo maneno hatutaki, tunaewana?

Mfano (1) ni kauli kutoka kwa mlezi wa makandidati wakati wa mafunzo kwa walelewa. Maswali ya mlezi huyu yanamtoa mlelewa katika hali ya kujibu swali kutoka kwa mlezi kuhusu kinachozungumziwa ambacho ni kuishi kama kundi moja na kuepuka kujipendekeza kwa walezi. Matumizi ya dhamira ulizi yanambainisha mlezi kama mwenye nguvu na mamlaka kuliko walelewa. Matumizi ya dhamira ulizi, sio muhimu tu kwa kutafuta ni mawazo gani yanatiliwa mkazo au yasiyotiliwa mkazo katika usemi fulani lakini katika kudhihirisha jinsi watu wanavyojitambulisha na kujipatia nafasi katika usemi husika.

Lugha huundwa kwa namna inavyotumika katika mawasiliano na kuweza kuonyesha mahusiano yanayokuzwa baina ya wazungumzaji kama ilivyo kwa walezi na walelewa kama anavyoeleza (Wodak, 2001). Uundaji huongozwa na majukumu ya kijamii na mahusiano yaliyomo kati ya washiriki katika mazungumzo na pia majukumu ambayo lugha inatekeleza katika mahusiano kupitia kitenzi katika kishazi (Halliday 1985, 1994, 2004). Kitenzi ndicho muhimu katika kueleza jukumu la kishazi. Kishazi, kwa kutegemea aina ya kitenzi kilichotumika, kinaweza kutumika kuyatekeleza majukumu kama kutoa ujumbe au maelezo, kuonya, katika kujua jambo au kuuliza, kutaka jambo litendeke, kukemea, kusifu, kuonyesha hisia fulani na kadhalika. Uhusiano kati ya lugha na wazungumzaji hautenganishiki kwa kuwa lugha ni zao la jamii katika mahusiano. Kila matini inayozungumzwa huwa kifaa cha kumfunza mzungumzaji kuhusu mazingira yake na jinsi mhusika anavyoyakabili katika harakati za kutekeleza majukumu mbalimbali ya maisha. Lugha kama ilivyo kwa jamii ya watawa hutumiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwemo kutoa mafundisho yanayomweka mlezi katika kiwango cha juu kimamlaka kutokana na ujuzi alionao wa kitaaluma na mlelewa katika nafasi ya chini.

Mfano ufuatao uadhihirisha mahusiano haya hata zaidi.

2. Niliwaambia mfano gani asubuhi? Wa wakimbizi, mnakumbuka? Ndio, kama unakimbia mita mia moja lazima uanze kwa bidii, kwa bidii zaidi ili uweze kuwa wa kwanza pale. Sasa leo tumeanza mita mia moja, usikubali kubaki nyuma. Sisi na wale wengine sasa tunapeana vijiti, mnajua kupeana vijiti? Ndio, sista. Kwa vijiti yule anayeanza kukimbia anakimbia namna gani? Polepole? Hapana, ukikimbia polepole utaweza? Hapana, si utafanya timu yako ifeli? Ndio. Tuwe tayari kupokezana kijiti kwa sababu sisi sote tunataka ushindi, shirika la Yosefu liinuke, tusiaibishe shirika la SSJ lianguke.

Mlezi wa makandidati katika (mfano 2) anaitumia lugha na kuingiza katika tukio la mazungumzo uelezaji wake wa maoni kuhusu maisha ya utawa pamoja na kuuliza maswali kwa walelewa (Halliday, 1971). Jambo hili linambainisha kuwa na mamlaka kuliko walelewa, na pia anaonyesha uhusiano anaouweka kati yake na msikilizaji; na kwa njia ya pekee nafasi ya mawasiliano anayoipanga ya kuuliza maswali. Mlelewa anadhihirika kama mwenye jukumu la kuyajibu maswali kwa jibu 'la' na 'ndio sista' hivyo kuadhihirisha umuhimu wa namna katika kuangalia mahusiano ya kimamlaka. Uchunguzi unadhihirisha pia mikakati ya matukio ya matumizi ya lugha inayotumiwa na wazungumzaji (walezi na walelewa) katika uundaji upya wa mahusiano ya kimamlaka hususan wakati wa malezi katika usemi kwenye kishazi.

Lugha hufungua na huweza kuwaweka binadamu katika viwango tofauti vya maisha kama viongozi, walezi na walelewa kama ilivyo katika nyumba za kitawa na kudhihirisha itikadi zilizomo kwa ukubalifu wa mawazo ya (Chilton, 2004) ambapo kuna ngazi mbalimbali za uongozi na utawala zinazodhihirisha mamlaka yaliyoko. Katika maisha ya kitawa kuna msamiati maalum unaotumika na unaochangia kutoa utofauti wa kingazi ulioko kama vile *Mama Mkuu*, *Mlezi*, *Sista Mshauri*, *Mkubwa wa Nyumba* na *Mkubwa wa Mwezi*. Lugha ndiyo inayotumika katika kutoa ngazi hizi za kimamlaka na utawala. Dhana kuwa walelewa sharti wazielewe na kutambua ngazi hizi zinatoa utofauti katika mahusiano kwenye nyumba hizi za malezi na kuwatoa walezi kama walio na mamlaka zaidi dhidi ya walelewa. Aghalabu walelewa hutumia ngazi hizi kihonorifiki wanapokuwa wanatagusana ili kuonyesha heshima lakini pia kuonyesha uwezo na mamlaka.

### **Namna katika Kishazi**

Kulingana na Halliday (1985), matini ya kisarufi ambayo hutumiwa kama msingi wa uchanganuzi katika Sarufi Amilifu Msonge ni kishazi. Kishazi kimetambuliwa kuwa kipashio kidogo kwa mujibu wa Crystal (1985) na Radford (1997) katika sarufi ambacho kinaweza kuchanganuliwa katika muktadha wa mawasiliano. Kwa hivyo basi namna inaweza kujidhihirisha kwa aina mbalimbali katika kishazi, kwa mfano kupitia vitenzi, kivumishi na aina fulani za unominishaji. Namna inatumiwa kutoa mitazamo na hali ya kujiamini kwa mzungumzaji kuhusu kauli yake.

Fowler (1985) anatoa orodha za kuelezea kuhusu kategoria hizi. Kwake, namna inajitokeza kwa kishazi kupitia idadi ya miundo ya kisarufi kama vile vitenzi visaidizi vya hali, vitenzi leksika na kadhalika. Namna isiyotambulishwa inaelezewa kupitia hali zilizo wazi kama vile lazima, anaweza, unaweza, naweza, huenda, nitaweza, ninge, ningali, inapaswa na kadhalika. Maana inayobebwa na hali hizi hutofautiana kutegemea muktadha kama inavyobainika katika mifano ifuatayo ya kauli tofauti kutoka kwa walezi mbalimbali.

3 *Lazima* kula kile kimeandaliwa, hakuna sitaki hiki, sitaki kile.

Katika mfano (3) ambao ni kauli ya mlezi wa mapostulanti, kitenzi kisaidizi cha hali *lazima* kimetumika kudhihirisha *wajibu* wa walelewa wa kula chochote kilichoandaliwa bila kuchagua. Muktadha huu unamtoa mlelewa kama aliye chini ya mamlaka ya mlezi na kutompa uhiari wa kutenda analopaswa kutenda.

4. *Lazima* sasa mwe mnajuana, ama, si ndio?

Mfano (4) ni kauli ya mlezi wa manovisi, ambapo *lazima* imetumika kuonyesha *uwezekano* wa manovisi kuwa wanajuana wao kwa wao. Uwezekano unadhihirika pia katika mfano (5) kupitia

maneno ya mlezi wa makandidati anayeonyesha uwezekano wa mlemelewa kupewa nafasi ya kuongoza shule na pia kupewa nafasi ya kuongoza katika jumuiya ya walelewa kama kiongozi wao. Mamlaka ya kimahusiano yanadhihirika kupitia maneno ya mlezi anayedhihirika kuwa na mamlaka ya kiujuzi dhidi ya mlemelewa.

5. *Huenda* ukapewa kuongoza shule, *huenda* usiwe kile unatamani, ndio, *unaweza* kwenda jumuiya ukapewa kuongoza, eee, hayo ndiyo maisha yetu.

Kauli ya mlezi wa makandidati katika mfano (5) kupitia kitenzi kisaidizi cha hali *huenda* kinachoonyesha *uwezekano* na kitenzi cha hali *unaweza* kinachoonyesha kupewa *ruhusa* ni mambo ambayo yanamfanya mlemelewa kuonekana kama mwenye mamlaka ya kumpa nafasi na ruhusa ya kuongoza wengine. Mfano (6) pia unaonyesha upeanaji wa ruhusa kupitia kitenzi kisaidizi cha hali *unaweza* kutoka kwa mlezi kwa mlemelewa ya kwenda na mlemelewa mwingine kanisani wakati wa kusali.

6. Rafiki *unaweza* kwenda naye kanisani kumsalimu Yesu badala ya kufanya yasiyopaswa kwenye jumuiya.

Hali ya kutoa *ruhusa* inadhihirika katika mfano (6) kupitia kitenzi *unaweza* ambayo ni kauli ya mlezi wa manovisi. Vitenzi visaidizi hivi vya hali vinaonyesha *uwezekano* wa majukumu ya mlemelewa katika siku za usoni. Kreidler (1998) anaeleza kuwa namna ya kiutambuzi inahusu uwezekano, hali ya kuwa au kutowezekana kwa kauli fulani. Ni namna inayohusu utathmini na hukumu ya mzungumzaji kuhusiana na kiwango cha kujiamini cha ujuzi wa kauli. Inafanya kazi kuelezea au kutathmini ufafanuzi wa uhalisia katika utekelezaji wa majukumu ya uzungumzaji. Ni aina ya utambulishi wa kisarufi unaoonyesha uamuzi wa mzungumzaji unaotokana na ujuzi wake wa uwezekano, uelekeo au uhakika wa kauli inayoelezewa katika sentensi (Langacker, 1991). Jambo linalojitokeza pia kutokana na kauli ya mlezi wa makandidati katika mfano (7) katika kitenzi kisaidizi cha hali *anaweza* kinachoonyesha uwezo kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao;

7. Kwa hivyo, tuwe na msimamo, kila mtu aweke msimamo wake na msimamo wetu ni Kristu, angalieni yule Yesu msulibiwa, daima yuko tayari kutungojea wewe na mimi, tumwendee, tumlilie na hakuna sala inapita bure. Hakuna *anaweza* maisha haya bila Yesu.

8. Kwa hivyo *unatakiwa* kuwa imara, shujaa, mwenye msimamo na *unaweza* kufanya uamuzi wa mambo, uamuzi ufao na watu watakutegemea.

Mfano (8) kutoka kwa mlezi wa makandidati unaonyesha maana inayodhihirisha uwezo wa kufanya uamuzi. Mifano hii inawatoa walezi kama wenye mamlaka kupitia matumizi ya vitenzi visaidizi hivi vya hali dhidi ya walelewa ambao hawawezi kwa mfano kumwambia mlezi *unaweza* ambayo itakuwa kinyume na matarajio ya kitaasisi ya maisha ya utawa. Kitenzi kisaidizi cha hali *unatakiwa* katika mfano (8) kilicho katika dhamira arifu kinambainisha mlezi kama mwenye mamlaka ya kuwaarifu walelewa wanalopaswa kulitenda. Katika mifano (3) hadi (8) kunadhihirika kauli tofauti kutoka kwa walezi mbalimbali. Kauli zinadhihirisha matumizi ya vitenzi visaidizi vya hali *lazima*, *unaweza*, *anaweza*, *huenda* na *unaweza*. Maana zake zinatofautiana kulingana na muktadha.

Makundi ya walelewa hata hivyo katika nyumba za malezi wanatumiwa katika kuendeleza taasisi ya watawa na kutazamwa kama kizazi cha kesho. Walelewa wanatumiwa na walezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kufuga wanyama ili kuweza kukidhi mahitaji kama vile kupata chakula, fedha na kadhalika. Hali hii linajitokeza kama njia ya ubishi usio wazi kupitia jinsi wanavyoitumia lugha wakati wa shughuli zao kama inavyodhihirika kwenye mfano ufuatao wa (9).

9. Mlemelewa mkandidati akimwelezea mlezi yaliyotokea wakati wa shughuli za kikazi:

Vile anavyonijibu hata mimi huwa nanyamaza na yeye huwa ananyamaza. Sijui alipeleka wapi mayai...na akaja hapa ikawa kama ni kugombana kati yake na mimi. Ilipofika wakati wa tathmini ya mwezi uliopita, akaja na hiyo hoja vile ninavyojibu na vile alivyonijibu. Pia, *huenda* siku ya kunitoa pale kwa kuku ndio ikaleta mambo mengi na tulikuwa tunabadilishana maneno na sijui kama alichukua hayo mambo akasema kwamba mimi ndiye

niliyeandika ile barua kwa sababu aligombana na mimi...*unaweza* kumuuliza sista yuko hapa...*nataka* umuulize sista mimi sina shida naye.

Katika mfano (9) ambao ni kauli kutoka kwa mlelewa mmoja ambaye ni mkandidati, inadhihirika wazi anafanya kazi kwenye sehemu wanakofugwa kuku. Kauli hizi zinadhihirisha matumizi ya mlelewa huyu ya lugha ambapo maneno yake yanaonekana kuwa na ukali, anatumia sentensi ndefu, maneno mengi na kuonekana kumwelekea mlelewa mwenzake. Mukadha unamfanya mlelewa anayeongea kudhihirika kama aliye na mamlaka kwa mlelewa mwenzake na kudhihirisha ubishi kwa kuwa walelewa wanafaa kuwa katika kiwango sawa na wenzao. Lugha inamtoa mlelewa kama aliye na mamlaka yasiyokuwa wazi na yasiyotarajiwa katika hatua za malezi.

Hali hii inadhihirika katika nyumba ya malezi ambapo walelewa wanaiweka wazi kama njia ya ubishi katika miktadha yao mbalimbali wakati wa mazungumzo. Matumizi ya kitenzi kisaidizi cha hali *huenda* kinaonyesha *uwezekano* ambayo ni njia isiyo wazi ya ubishi kwa kumpa mlelewa nafasi ya kutoa kauli asiyokuwa na uhakika nayo na inayombainisha kama mwenye mamlaka kupitia kauli yake. Pia kitenzi kisaidizi cha hali *unaweza* kinadhihirisha ubishi kwa kuwa mlelewa ni kama anampa mlezi *ruhusa* ya kuuliza mlelewa mwenzake yaliyotokea hivyo kuonekana kama aliye na mamlaka dhidi ya mlezi.

### Namna katika Vitenzi Visaidizi vya Chagizo

Namna inaweza pia kuelezewa kwa chagizo kama vile *hakika*, *hasa/kabisa*, *labda*, *haikosi*, *daima*, *aghalabu*, *pasipo shaka*, na kadhalika kama inavojitokeza katika mifano ifuatayo:

10. *Ndio*. Kutoka sasa tunza wito wako sawa? *Ndio*. Ungepata nafasi saa hii ungeweza kuondoka? Najua la *kabisa*! Endelea basi na wito wako. Sawa? Ungepata shirika nyingine si *labda* ungeweza kwenda huko? Lakini sasa uko hapa. Endelea ndipo umeitwa. Sawa? Mlelewa A umekaa miaka sita mkiwa na mlelewa B mbona hiyo miaka hamkuolewa basi, Mngekuwa mmeolewa basi? *Haikosi* mngekuwa na watoto.
11. *Ndio*, hayo mambo hatutaki tutawagawa katika shughuli mbalimbali tusikize, hapa watu si wa kabila moja, sitaki kusikia ati kwa sababu wewe una watu wa kabila lako *labda* hao tushike hivi, haipaswi katika haya maisha.

Matumizi ya *labda* katika mifano (10) na (11) yanaonyesha kiwango fulani cha kuwa na uhakika. Mfano wa (10) ukionyesha kiwango cha uhakika kuwa iwapo mlelewa angekuwa amepata shirika lingine huenda angekuwa amejiunga nalo na hivyo kutojiunga na shirika la masista wa Mtakatifu Yosefu. Nao mfano (11) ukionyesha uhakika wa walelewa kushika wanaloambiwa jambo linalotekelezwa kupitia wakati uliopo. Mukadha hii inadhihirisha mahusiano yaliyo na mamlaka kutoka kwa walezi kwa walelewa.

### Ubainikaji wa Namna kupitia Vitenzi Leksika

Vitenzi leksika vingine vinaweza kuelezea hali kama vile *ruhusu*, *omba*, *amini*, *amuru*, *zuia*, *thibitisha*, *kisia*, *ahidi*, *onya*, *shauri*, *stajabu*, *tamani*, *fikiria*, *dhani* na kadhalika kama ilivyo kwenye mifano ifuatayo;

12. *Ndio*, kwa hivyo, hapa sitaki vikundi vitano ama sita ama mbili, na ni vile niliwaambia jana itakuwa aibu umebeba sanduku, watu wamekuona ukitoka kwenu na sanduku na watu wakakusindikiza kwaheri na baada ya siku kidogo *naomba* nini, sijui sista, sijui nasikia, sijui nini, wewe ulitafakari, ulikuwa na muda wa kutafakari.
13. Nawe umefika hapa sasa unataka kumpura mawe sista mlezi ndio uondoke. Ni kitu gani ambacho *umefikiria* kukihusu? Kwa hivyo *dhamini* wito wako, ulinde wito wako.

Katika mifano (12) na (13) ambazo ni kauli zinazotoka kwa mlezi wa makandidati, maneno ya mlezi yanayowapa walelewa motisha wa kuyashika maisha waliyoyakumbatia bila kuangalia nyuma kwani ni jambo walilolifikiria kabla ya kufanya uamuzi. Hayo yanadhihirika kupitia matumizi ya vitenzi leksika '*naomba*', '*umefikiria*' na '*dhamini*' vinavyoashiria sifa za kitawa anazostahili kuwa

nazo mlelewa kuifikia ndoto yake. Mifano ikitoa hali inayodhihirishwa na kitenzi leksika cha *kudhamini* kinachoashiria hamu ya mlelewa ya kulifikia lengo la maisha.

14. Najua *mnatamani* kuwa watawa.

15. Tumekuja kutafuta *utakatifu*, tumekuja *kutamani ukamilifu*, tunapaswa kuwa wanawake wa sala, lazima tufanye kazi pamoja na Yesu, tufanye chochote tufanyacho naye, hata unaweza kumkaribisha Yesu unapoenda kulala akulinde na kuwa nawe....

Mfano (15) ni maneno yanayotoka kwa mlezi wa manovisi kama ilivyo katika mfano wa (14). Maneno '*mnatamani*,' '*utakatifu*' na '*ukamilifu*' yanaonyesha ari anayopaswa kuwa nayo mlelewa katika kuyatekeleza anayofunzwa na hivyo zao la utakatifu ni maisha mema ya mlelewa na hatimaye sista wa kesho. Hata hivyo maneno haya yanaweza kuashiria hali inayodhihirishwa na kitenzi leksika cha *kutamani* maisha ya kitawa mlelewa anayoyatamani kuyaishi baadaye ili awe na raha na hatimaye afikie lengo lake maishani la kumtumikia Mungu.

### **Ubainikaji wa Namna Kwenye Vitenzi Leksika Visaidizi vya Hali**

Namna inaweza pia kuelezwa kupitia vitenzi leksika visaidizi vya hali kama vile *karibia kuwa, kuwa na uhakika wa, kuweza kuwa, elekea kuwa, tazamia kuwa, shurutishwa kuwa, kupaswa kuwa, kuwa na uwezekano kuwa* na kadhalika.

16. Mlelewa X: Kulingana na mimi vile nimeona huo muda tumekuwa hapa, katika maisha haya *tunashurutishwa* kufuata sheria za shirika la masista wa Mtakatifu Yosefu na vile tunafunzwa ni kama ukilazimishwa au kufuata vile wengine wanafanya huenda usiwe na raha. Hivyo tujaribu kila mtu awe na msimamo wake wa maisha bila kusukumwa.

17. Tujaribu tuwe na unyenyekevu na kujifunza kusema sista ni mimi nilifanya hiki ili kufanya maisha yetu yawe rahisi, wakati tukikosa tuwe wanyenyekevu na tukifanya shughuli zetu *tunapaswa kuwa* waangalifu vile tunafanya.

18. Kuna watu wanakula maganda na kuacha tu hapa. Sista akiyakuta hatafurahia na ataturekebisha tu. Tufanye vile *tunatakiwa* kufanya mbele ya Mungu.

Mifano (16), (17) na (18) ni kauli kutoka kwa walelewa wanapokuwa peke yao. Usemi wao unadhihirisha lile wanalopaswa kulitenda ili kuweza kuyafurahia maisha yao yanayowaandaa kuishi vizuri baadaye. Kupitia matumizi ya lugha wanadhihirika wenye mamlaka ya kuongozana wenyewe kwa wenyewe na kusaidiana kushika yanayofaa. Kauli zinabainisha hali ya namna ya matamaniao na hamu waliyonayo maishani na kudhihirisha mamlaka yao ya kitaasisi.

19. Utii ndio unatufanya watawa *tuweze kuwa* na mwelekeo bora wa utawa katika nadhiri zote tatu; usafi wa moyo na wa mwili, umaskini na utii, zote zitabebwa na utii na usingojee ati uje kutii mambo makubwa makubwa yale madogo hata kama unaambiwa na dada zako, niliwaambia asubuhi kama ni ya ukweli ufanye na kama si ya kweli usifanye nini?

20. Kila mmoja wetu lengo lake ni *kutazamia kuwa* mtawa au sio? Ndio. Si tunataka?

Mfano (19) na (20) ni maneno yanayotoka kwa walezi wa manovisi na mapostulanti. Maneno yanaonyesha hamu ya wajibu na matamaniao ya walezi na walelewa katika maisha wanayoyaishi pamoja na hukumu kama wazungumzaji kulingana na kiwango cha kujiamini kupitia kauli wanazozitoa. Walezi wanahimiza walelewa kuwajibikia maisha yao ili hatimaye wafikie lengo lao maishani la kumtumikia Mungu.

### **Namna katika Kishazi chenye Kivumishi**

Namna inaweza kutambuliwa katika kishazi chenye kivumishi kinachofuatwa na kitenzi kisoukomo au kishazi cha kuwa. Vivumishi vinavyotumiwa kuelezea namna ni kama - *a hakika, yakini, - kufaa, yawezekana* na kadhalika.

21. Mimi *nina hakika kusema kuwa* nitakuwa mtawa katika shirika hili la masista wa Mtakatifu Yosefu. Nyinyi ngojeni tu mtashangaa nikifurahia kuvaa shela. Miaka miwili tu... Mungu anaweza yote.

22. Mimi naona yawezekana yakini kupewa nadhiri mwaka huu... achene kucheka mimi niko serious. Kwani mnataka kurudishwa nyumbani? Hapo sipo mimi *Nina hakika kuwa yawezekana kupewa* sista hapa singatuki mimi hata iweje...

Hizi ni kauli za walelewa ambao ni mpostulanti na mnovisi. Kishazi '*nina hakika kusema kuwa*' na '*yawezekana kupewa*' vinadhihirisha hali ya namna inayowatoa kama wenye uwezo na nguvu kimamlaka kwa yale wanayoyasema. Maneno yao yakidhihirisha uwezekano wa wanayoyasema.

23. Huwezi kusema kuwa hivi ndivyo nilivyo, hapa si mahali pa kusema hivi ndivyo. Ndio. Inabidi. Ndio *inafaa kuwajibika* na kuwa *na uhakika* katika maisha ya mtu binafsi na kuweza kujitawala na kuwa na nidhamu. Ndio *yafaa kuwa* watu walio mfano bora katika jamii.

Kauli hii inatoka kwa mlezi wa makandidati katika mafundisho ya maisha ya utawa. Katika mfano huu (23) mlezi anawahimiza wawajibikie maisha na wachukue jukumu kuhusu maisha waliyoyachagua.

### **Kishazi chenye Wakati Uliopita Hali ya Kuendelea Katika Kubainisha Namna**

Namna inaweza pia kuelezwa katika kishazi chenye wakati uliopita hali ya kuendelea ikifuatwa na kitenzi kisoukomo au kishazi cha kuwa. Vitenzi vya wakati uliopita hali ya kuendelea ni kama *ruhusiwa, tambulishwa, thibitishwa, takiwa* na kadhalika kama inavyojitokeza kwenye mifano inayofuata.

24. Msichoke kusikiliza haya najua mmeambiwa tangu ukandidati. *Inahitajiwa* mlelewa atii maishani. Sawa.

Kauli hii inatoka kwa mlezi wa manovisi katika mafundisho ya maisha ya utawa. Katika mfano huu (24) mtendaji ambaye ni kiima hadhihiriki lakini tendo la kutoa mafunzo kwa walelewa linaelezwa kama la hali ya kuendelea katika kuwafunza ili hatimaye wawe watawa wema. Kitenzi cha wakati uliopita hali ya kuendelea *inahitajiwa* kinatumika kudhihirisha namna. Katika mfano huu, mlelewa anadhihirika katika kauli ya kutendewa inayomwonyesha kama kiima anayethirika kwa kupokea tendo la malezi hivyo kumfanya anayemlea ambaye ni mlezi kuwa na mamlaka dhidi yake. Hata hivyo wenye jukumu la kuwaandaa walelewa ambao ni watendaji ni walezi ambao hawajatajwa katika mfano huu. Jambo hili linajitokeza pia kutoka kwa kauli ya mlezi wa makandidati kwenye mfano ufuatao kupitia matumizi ya vitenzi vya namna *tunatakiwa* na *kukaribia*.

Hebu tuangalie mfano zaidi hapa chini,

25. *Tunatakiwa* kuchukuliana sisi sote sawa, si ati kwa sababu wewe ni Mtaita unataka *kukaribia* sista mlezi kwa kuwa ni mtaita na unajua kuna tatizo lingine; kuna watu ambao wakikaa katika kikundi kama hiki wanataka kupendwa... si mwawajua?

Katika kauli hii ya mlezi katika mfano (25) wa makandidati, kitenzi *tunatakiwa* kinawaweka walezi na walelewa katika kiwango sawa cha kuathiriwa na tendo la wanachotakiwa kufanya. Ujumlishaji huu unatoa ubishi pale unapoweka mlezi na mlelewa kama walio na wajibu wa kutekeleza jambo la kuchukuliana wote kwa usawa. Hili ni kinyume na matumizi ya kitenzi *kukaribia* kinachomlenga mlelewa kama mwathiriwa wa tendo la kutaka kuwa karibu na mlezi hivyo kumtoa kama aliye chini katika malezi na anayemtegemea mlezi sana ili kufikia hatima yake. Vitenzi vinadhihirisha wakati uliopita hali ya kuendelea hivyo ni mambo wanayopaswa kuyatenda wanapoendelea na malezi yao.

### **Ubainikaji wa Namna Katika Kishazi chenye Nomino**

Uwezekano mwingine wa kutambua namna ni kupitia kishazi kinachoanza na kiwakilishi nomino *ni* au kidhanaishi *kuna* kikifuatwa na nomino na kishazi cha kuwa. Nomino zinazotumiwa kuonyesha namna ni kama vile *jambo la lazima, nafasi, uwezekano, uelekeo, welekeo, uhakika, uamuzi* na kadhalika. Haya yanadhihirika katika mifano ifuatayo kutoka kwa walezi mbalimbali. Hebu tutazame mifani ifuatayo:



26. Ndio, ni *wajibu wetu kuwa* na moyo wa kumtumikia Mungu na kanisa haijalishi kazi unayoifanya, lazima uwajibike kwa kazi ya kanisa kwani huo ndio wito wetu wa kwanza.
27. Ndio. Huwezi kusema kuwa hivi ndivyo nilivyo, hapa si mahali pa kusema hivi ndivyo nilivyo, kama ninavyowaambia kila siku, ukitaka kuwa mtawa na mwanamke mtawa mzuri *jambo la lazima* ni kubadilika, *kuna uwezekano kuwa* usipobadilika na kubadilisha matendo yako mabaya uliyokuwa nayo kabla *huenda usiwe* mtawa mwema, mnaelewa?
28. *Nina uhakika kuwa* mliyatafakari haya yote mkiwa nyumbani kabla ya kufanya *uamuzi*.
29. Tumekuja kutafuta utakatifu, kutafuta ukamilifu, tumekuja kuwa wanawake wa sala. Inabidi tufanye yote na Yesu, kumtembelea Yesu, kukaa na Yesu, kufanya chochote tutakachokifanya na yeye, hata kumwalika unapolala na kumwomba akupatie ndoto nzuri, usingizi wa amani, mwambie Yesu, mwambie nimefanya kazi kwa bidii leo na nataka usingizi mzuri, utalala vizuri, utalala kwa amani kwa sababu *unajua kuwa kuna* mtu anakuunga mkono, Yesu yuko kando yako.

Semi hizi za walezi tofauti zinadhihirisha hali ya lazima na wajibu wa kuwa na moyo wa kuzingatia linalofaa na hivyo kudhihirisha namna kupitia vishazi vya nomino.

### **Namna katika Kishazi cha Masharti**

Kishazi cha masharti kinaweza kubeba maana ya namna kuonyesha uwezekano. Kama sharti *limetimizwa, lawezekana, kuelekea* au *hakika kuwa* sharti lingine litafanyika.

30. Niliwaambia mfano gani asubuhi mwingine? Wa... Wakimbizi, mnakumbuka? Ndio, *Kama* unakimbia mita mia moja lazima uanze kwa bidii, kwa bidii zaidi ili uweze kuwa wa kwanza pale (Uwezekano).
31. *Kama* ulikuja kuwa mtawa fuata kile umekuja kufanya na ninawasihi usishikane na mtu akuelekeze visivyo, umekuja hapa mtu mzima ishi maisha yako (Uhakika).

Mifano (30) na (31) inadhihirisha uwezekano kama ilivyo kwenye mfano (30) na uhakika katika mfano (31). Vishazi hivi vinaonyesha uwezekano na uhakika wa jambo moja kufanyika likifuatiwa na lingine. Kuwa ili walelewa wafaulu sharti watimize matakwa fulani wakati wa hatua za malezi.

### **Hitimisho**

Utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi mahusiano na mamlaka yanavyobainika katika nyumba za watawa za kanisa Katoliki katika jimbo la Mombasa. Uchunguzi umedhihirisha namna kujieleza na ubainikaji wa mahusiano ya kimamlaka katika nyumba za watawa za malezi kupitia matumizi ya lugha hutokea. Umebainisha kuwa mahusiano ya kijamii yanaweza kuelezwa kupitia namna kwa kuzingatia vitenzi visaidizi vya hali, vitenzi leksika, kishazi chenye nomino na kadhalika na hivyo kusaidia kuelewa kuwa kuna dhana zinazokaziwa na zisizokaziwa kuhusu mamlaka. Majukumu ya kiuamilifu yanayohusu matumizi ya lugha katika kuelezea mahusiano ya jamii ya walezi na walelewa na ya mtu kibinafsi yamedhihirika na kudhihirisha kiwango cha mamlaka cha wazungumzaji mbalimbali. Dhamira ulizi imetumika kama njia ya kuonyesha kuwa, walezi na walelewa wanadhihirisha kiwango fulani cha mamlaka.

Kupitia matumizi ya lugha namna imejidhihirisha kupitia aina mbalimbali katika kishazi na sentensi na kutokana na namna kumedhihirika kauli za walezi na walelewa za wajibu na uwezekano. Namna inawaweka washiriki katika viwango tofauti kimazungumzo na kitaasisi hivyo kudhihirisha mamlaka yasiyo na usawa kwenye nyumba za malezi. Walezi wamejitokeza kama wanaotumia namna zaidi katika usemi hivyo kuwatoa wenye mamlaka dhidi ya walelewa. Kauli zao aidha kupitia namna zinadhihirisha uhakika, jukumu na wajibu wa kile wanachokisema kwa walelewa na wanatumia ulazima jambo ambalo ni nadra kwa walelewa kulifanya.

### Marejeleo

- Chilton, P. (2004). 'Metarepresentation, discourse and discourse spaces' in Marques, M. Aldina (Toleo), *Práticas de investigação em Análise Linguística do Discurso - Actas do II Encontro Internacional de Análise Linguística do Discurso*, Cehum, Braga.
- Crystal, D. (1985). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics* (Toleo la nne). Oxford: Blackwell.
- Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. London: Longman.
- \_\_\_\_\_ (2000). *Language and Power* (Toleo la pili). New York: Longman.
- \_\_\_\_\_ (2010). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study Language*. (Toleo la pili). U.K: Longman.
- Francis, G. & Kramer-Dahl (1992). "Grammaticalizing the Medical Case history." Katika, Toolan, M. (Mhariri), *Language Text and Context: Essays in stylistics*. London: Routledge Uk. 56-92.
- Endley, M. J. (2010). *Linguistic Perspectives on English Grammar: A Guide for EFL Teachers*. Hanyang: Information Age Publishing.
- Fowler, R. (1985). *Power*. In T. A. van Dijk (Mhariri), *Handbook of Discourse Analysis, Vol. 4*. London: Academic Press, Inc. Uk.61-82.
- Halliday, M.A.K. na Hassan, R. (1976). *Cohesion in English*. London: Longman.
- Halliday, M. A. K. (1971). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.
- \_\_\_\_\_ (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.
- \_\_\_\_\_ (1994). *An Introduction to Functional Grammar* (Toleo la pili). London: Edward Arnold.
- \_\_\_\_\_ (2004). *An Introduction to Functional Grammar* (Toleo la tatu). London: Edward Arnold.
- Kreidler, W. C. (1998). *Introducing English Semantic*. London: Routledge.
- Langacker, R.W. (1991). *Foundations of Cognitive Grammar Vol. II Descriptive Application*. California: Stanford University Press.
- Radford, A. (1997). *Syntactic Theory and the Structure of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Wodak, R. (2001). "What CDA is about – a summary of its history, important concepts and its developments" Katika, Wodak R & Meyer, M. (Wahariri) *Methods of Critical Discourse Analysis*. London: Sage Publications Ltd. 1-13.